

HALMASHAURI YA MJI WA MBULU

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)

Unapojibu tafadhali taja:
Simu Na. +255 271 2533331
Fax 255 271 2533330
Mbulu-Manyara



Mkurugenzi wa Mji
Halmashauri ya Mji wa Mbulu,
S.L.P. 164
Mbulu/ Manyara

CIRCULAR RESOLUTION

20/10/2021

Dokezo la kutoa idhini ; No 2.

**Wajumbe wa bodi ya zabuni
Halmashauri ya Mji wa Mbulu.**

Kwa Mujibu wa kifungu cha 58 (1) cha kanuni za manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013 (GN. NO. 446, 2013) kina sema kuwa maamuzi ya tenda Bodi yanaweza kufanyika hata bila ya kufanya kikao cha tenda bodi kwa kutumia "Circular Resolution".

Kwa Mujibu wa kifungu cha 58 (2) cha kanuni za manunuzi ya umma ya Mwaka 2013 (GN. NO. 446, 2013) kwamba kwa kuwa kikao cha tenda Bodi hakitakaa wajumbe wa Bodi ya zabuni watasambaziwa nyaraka zinazohusiana na manunuzi husika ili kutoa maamuzi ya idhini ya manunzi hayo kufanyika.

Quoram

Kwa Mujibu wa mwongozo (guide line; version NO; PPRA:GL/05/2020/TBCR) wa PPRA uliotolewa mwezi Mei, 2020 umeelekeza kuwa nusu ya wajumbe wa bodi ya zabuni wanaweza kuidhinisha manunuzi kufanyika.

Maelezo ya Manunuzi yanayofanyika.

Halmashauri ya Mji wa Mbulu imepokea fedha Tshs **110,000,000.00** na **90,000,000.00** nyumbaya mtumishi ambazo hazikuwepo kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVICO19. Fedha hizi ni kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 20ya shuleza sekondari na madarasa 8 ya shule shikizi za msingi.

Gharama za Miradi

Halmashauri inatarajia kujenga madarasa 28 ambapo kila darasa moja litagharimu kiasi cha Tshs 20,000,000.00 na kufanya gharama ya ujenzi wa madarasa kuwa Tshs 560,000,000.00, kituo cha afya Kainam kitagharimu kiasi cha tshs 250,000,000.00 ikiwa ni fedha za awamu ya kwanza na ujenzi wa jengo la huduma ya dharula Hospitali ya Mji wa Mbulu litagharimu kiasi cha tshs 300,000,000.00.

Mwenyekiti, kwa kuwa fedha hizi hazikuwepo kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022 kwa kikao hiki tunaomba idhini ya kuingizwa kwenye mpango wa manunuzi wa 2021/2022 ili fedha hii iweze kufanya kazi ya ujenzi wa miundombinu ya elimu na afya.

Kikao chako kinaombwa kutoa idhini ya kutumia njia ya force account kutekeleza miradi hii, kwa kuridhia kuundwa kwa kamati ya manunuzi, kamati ya Ujenzi na kamati ya mapokezi na ukaguzi kusimamia shughuli za manunuzi kuwa kufuata sheria na taratibu ili kukamilisha miradi hiyo.


Aidha kuridhia orodha ya mafundi na watoa huduma ya usambazaji wa vifaa vya viwandani na local materials ambao watahusika katika utekelezaji wa miradi hii.

Quotation ya manunuzi ya cement mfuko 5040 na Nondo 12mm BS pcs 1120 ziliwasilishwa kama ifuatavyo;

- Bulk Distributors Ltd (Arusha) anauza Cement mfuko mmoja Tshs 14,700/=
 - Simba Cement (Tanga) anauza Cement mfuko mmoja Tshs Tshs 14,750/=
 - Bulk Distributors Ltd (Arusha) anauza Nondo 12mm BS roll moja Tshs 23,260.01
- Kampuni ya Bulk Distributors Ltd imepitishwa kama mzabuni wa vifaa vya viwandani.

Orodha ya Wajumbe wa Bodi ya zabuni ya Halmashauri ya Mji walioridhia taratibu za manunuzi kwa mujibu wa sharia na taratibu zifanyike.

| S/N | Jina | Cheo | Approve/Disapprove | sign | Date |
|-----|-----------------------|--------|--------------------|-------------|------|
| 01. | Dr Christopher Nyaku. | Member | Agree | CA Iku. | |
| 02. | JOVIN DIDACE | member | Agree | [Signature] | |
| 03. | HILARY MAKWADI | MSUMBE | AGREE | [Signature] | |
| | | | | | |
| | | | | | |


.....
Chairman/Secretary